SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No. June 16

THAMANI YA NDANI YA KIFASIHI KATIKA FILAMU TEULE ZA KITAMADUNI

Simba Haji Gora
simbagora0@gmail.com
Baraza la Kiswahili la Zanzibar
Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Received: February 2025, Accepted: April 2025, published: June 2025
© SUMAIT University Journal 2025

Abstract: *This article examines the intrinsic literary value found in cultural films. The main argument of the article is to demonstrate that, despite literature being viewed primarily as entertainment, it can also be viewed in the way it is constructed to deliver that entertainment. Data were collected through the method of textual analysis by watching and analyzing the films. Axiological theory guided the data collection and analysis. The central question that led to the creation of this article was: what literary values can be found in selected films? Normally, critics focus on the form and themes in literature in a way that is superficial, but they do not consider how these elements build literary value. The intrinsic values identified include the use of figurative names, depiction of settings, character portrayal, and narrative structure.*

Ikisiri: *Makala hii imechunguza thamani ya ndani ya kifasihi inayopatikana katika filamu za kitamaduni. Hoja kuu ya makala ni kudhihirisha kuwa burdani inayopatikana katika fasihi hutokana na namna fasihi hiyo ilivyoundwa. Hali hiyo ndio inayoonesha thamani yya ndani ya fasihi. Data zimekusanya kupitia mbinu ya uchanganuzi matini kwa kuzipitia filamu na kuzichambua. Nadharia ya aksiolojia ndio iliyoongoza katika ukusanyaji wa data na uchambuzi. Swali muhimu lililoongoza upatikanaji wa makala hii ni; ni thamani zipi za kifasihi zinazopatikana katika filamu teule. Matokeo ya swali hilo ni kwamba Thamani ya ndani iliyobainika ni pamoja na uitaji wa majina kimajazi, usawiri wa mandhari, utomeleaji na utenguzi.*

Keywords: ***Filamu, muvi, michezo ya kuigiza, aksiolojia na thamani ya filamu.***

1.0 Utangulizi

Thamani ya fasihi inafafanuliwa kwa mitazamo tofauti kutegemeana na mitazamo ya wataalamu mbalimbali. Mitazamo hiyo inaweza kujitofautisha kati ya kundi moja na jingine. Kwa mfano, **[16]** anaigawa thamani ya fasihi kwa kutumia mikabala miwili. Mkabala wa kwanza ni ule wa kimajumui, ambao unatazama usanii uliomo ndani ya kazi ya sanaa kwa kutazama mvuto wa utengenezaji wa sanaa husika kwa kutumia lugha teule na yenye kutoa burudani kwa msomaji. Pili, fasihi inaweza kuwa na thamani ya kiujumi. Msanii anapoweza kuwasilisha ujumbe kwa kutumia njia mbalimbali zinazoilenga jamii basi msanii ataonekana amefanikiwa kuonesha thamani ya fasihi. Akiendelea kutoa ufafanuzi wake **[16]** anasema, ni wazi kuwa fasihi hupimwa kwa kipimo cha kithamani kutokana na namna ya uwasilishaji wake au katika ujumbe uliomo kwenye kazi husika. Ingawa

maelezo yake ni ya kinadharia tu ila yamesaidia kututanabaisha kuwa thamani ya fasihi ni jambo la msingi ndani ya fasihi.

anazungumzia mitazamo ya wahakiki na waandishi wa kazi za fasihi katika msisitizo wa thamani ya fasihi kwa jamii. Anasisitiza kwa kusema, wahakiki wengi wa fasihi hawazingatii umuhimu wa thamani katika fasihi. Katika maelezo yake anaonesha jinsi thamani ya fasihi inavyoweza kuhusiana moja kwa moja na fasihi. Pia thamani hiyo inaweza kuhusishwa na maadili. Uzoefu wa uzuri na ubaya katika fasihi nao unaweza kutazamwa kama thamani ya fasihi. Thamani ya fasihi ni suala lililojadiliwa kwa muda mrefu na kusababisha kuwapo kwa mitazamo tofauti kutoka kwa wanafalsafa mbalimbali. **[4]**

Maelezo ya **[4]** katika kuitazama thamani ya fasihi yameonesha namna waandishi wanavyosisitiza thamani ya fasihi kama inavyoonekana katika kazi za kifasihi. Kupitia maelezo yake tumejifunza kuwa msisitizo wa thamani katika jamii ni jambo la msingi sana. Pamoja na maelezo hayo, bado hakutazama ni thamani ipi inapaswa kuwapo katika fasihi ya jamii fulani. Pia, hakuonesha ni kwa vipi thamani hiyo huwa inaibuliwa.

anabainisha thamani ya ujumi wa Kiafrika katika vipengele kadhaa ambavyo ndivyo vinatambulisha na kuathiri utamaduni na maisha ya Waafrika kwa sehemu kubwa. Vipengele hivyo vya kiujumi huambatana na umbo la ndani la kazi ya fasihi. Vipengele vilivyojadiliwa katika makala hiyo ni kuishi kwa ushirika, utu, utii na adabu, makusudio, ushababi, ukizinda, na imani za dini. Anaonesha kuwa kuishi kwa ushirika ni miongoni mwa vipengele vya kithamani kilichoelezwa na waandishi wa hadithi fupi. **[14]** anasisitiza kuwa mifumo iliyoundwa na watu kwa ajili ya kuiongoza jamii ikijadiliwa na waandishi wa fasihi huwa inalenga kuona kuwa fasihi hiyo inayo thamani ya kijamii.

Maelezo hayo ni muhimu kwa sababu yanaonesha wazi kuwa kila utanzu wa fasihi unaweza kuwa na thamani yake. Vilevile, yamebainisha kwa uwazi thamani za fasihi zinazopatikana katika kazi ya fasihi kwa kuiona jamii huwa ndio mwanzilishi, mwangalizi na mwelekezaji wa mienendo na masuala mbalimbali yanayopaswa kuwemo katika fasihi. Pia, mwanafasihi ndiye anayesadifu mfumo wa jamii kwa kuunasibisha na imani ya Miungu. Matakwa ya imani za dini kuhusu himizo la kufanya matambiko, miviga, ibada na sherehe kiushirika ni ushahidi kuwa mfumo huu una mizizi katika masuala ya kiimani. Hivyo, Waafrika walisisitiza maisha ya ushirika kama kanuni ya msingi ya maisha. Hivyo fasihi yoyote yenye misingi hiyo huwa ina thamani.

[3] wanafafanua thamani ya fasihi kwa kuigawa katika makundi kadhaa. Mosi thamani ya kisiasa: katika thamani hii anaona kuwa kazi ya fasihi inaweza kumsukuma mtu kuchukua hatua inayoweza kufichua dhuluma, kutoa sauti kwa wanaoonewa, kuwadhihaki mafisadi, na ikiwa inajaribu kuwashawishi watu au ulimwengu kuanza kutenda na kufikiria kwa njia yenye tija kwao. Pili, anafafanua thamani ya kitamaduni. Ikiwa kazi inashughulikia mitazamo, desturi, na maadili ya wakati wao au wakati mwingine, basi kazi hiyo hutazamwa kuwa na thamani ya kitamaduni. Tatu, anafafanua thamani ya kifalsafa kwa kujumuisha fasihi yenye kuchunguza kwa undani kuwapo kwa kitu, au maumbile na namna kinavyofanya kazi. Kazi ikijipambanua kwa mitindo hiyo huhesabiwa kuwa kazi hiyo ina thamani.

[6] anafafanua kwa kusema, thamani ya fasihi ni jambo lisiloepukika katika fasihi. Jambo hilo linakutana na kanuni zinazojulikana za uhakiki wa fasihi. Thamani hiyo inatokana na kuchunguza ujuzi alionao mwandishi, lengo la kazi, upekee wa ubunifu, uasili wa kazi za sanaa, athari ya masimulizi, kuishi katika nyakati zote, ubunifu unaotambulisha utamaduni wa kijamii, ubunifu unaotegemea soko, na kuchunguza tabaka lengwa. Maelezo ya **[6]** yanaweka vigezo msingi katika kuchunguza thamani ya fasihi. Vigezo hivi vinatoa nafasi ya kuona kuwa fasihi haiwezi kujikamilisha yenyewe bila ya kuwa na thamani.

Thamani ya ndani ya kifasihi hujumuisha ufundi autumiao msanii katika kusana kazi yake. Thamani hizo zinaweza kujitokeza katika matumizi ya lugha ya kisanii. Kanuni hii inasisitiza umuhimu wa lugha, taswira, na mtindo katika kujenga tajriba ya kusoma yenye maana na ya kufurahisha.

Kama ilivyo katika fasihi, thamani ya ndani ya kifasihi katika filamu inapimwa kwa jinsi vipengele hivi vinavyofanya kazi pamoja kuunda hadithi yenye maana na athari, bila kuzingatia mambo ya nje yatakayopatikana kupitia filamu. Vipengele vya ndani vya filamu vinachangia kutambulika kwa filamu kama kazi bora ya sanaa. **[2]** wanasema kuwa thamani ya ndani ya kifasihi katika filamu inahusiana na mbinu ya usimulizi, usawiri wa wahusika, mitindo ya kisanaa na mandhari vinavyohusiana na maadili ya kifasihi na uhalisia wa kijamii au kihistoria. Katika filamu ya *Matusi* na *Wali Wangu*, utafiti uliozalisha makala hii umebaini thamani ya ndani ya kifasihi katika vipengele vya usawiri wa wahusika kimajazi, utomeleji, utenguaji, na usawiri wa mandhari.

2.0 Methodolojia na Nadharia Iliyotumika

Data za makala hii zilikusanya kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini. Mbinu hii huchanganua matini mbalimbali kwa kupitia nyaraka, vitabu, kusikiliza sauti katika vyombo vya kunasia sauti au kuangalia video. Kwa vile makala hii imechambua filamu, mbinu ya uchanganuzi matini imekuwa ni faafu zaidi katika kukusanya data. Filamu ya *Matusi* na wali wangu zimetazamwa kwa utulivu na uangalifu wa hali ya juu ili kugundua taarifa za msingi katika filamu hizo. Uchunguzi huo umefanya kupitia mwongozo wa uchanganuzi wa matini.

Kwa upande mwingine, makala hii imetumia Nadharia ya Aksiolojia. Aksiolojia ni nadharia inayojihusisha na uchunguzi wa thamani ya kitu au mtu. Nadharia hii huhoji uzuri wa kitu. Jibu la swali hilo linabainika kupitia matawi mawili ya kifalsafa yanayoundwa na nadharia hii. Tawi la kwanza linahusu uzuri na ubaya wa kitu (ujumi). Tawi la pili linahusika na uainishaji wa maadili kwa kuchunguza kipi au lipi ni sahihi na kinyume chake. Aksiolojia ni nadharia inayojihusisha na nyanja mbalimbali za kifalsafa ambazo hutegemea sana dhana ya thamani, kama vile maadili, ujumi au falsafa za kidini. Kwa ujumla, Aksiolojia ni nadharia ya thamani na maadili ya meta (vitu vinavyoonekana). Hart (1971) anasema Nadharia ya Aksiolojia ilitumiwa kwa mara ya kwanza na Eduard von Hartmann mwaka 1887 na kuendelezwa na Paul Lapie mwaka 1902. Hata hivyo, tawi la utambuzi wa uzuri na ubaya wa kitu (ujumi) lilishatumiwa tangu miaka ya 1750 na mwanafalsafa wa Kijerumani, Alexander Gottlieb Baumgarten. Baumgarten aliasisi nadharia ya utambuzi wa uzuri na ubaya na kuanza kuitumia katika uchambuzi wa kifasihi. Pia, aliitumia katika kuandika na kuchambua fasihi za Kijerumani kabla ya Immanuel Kant kuitumia mnamo mwaka 1790.

Nadharia ya Aksiolojia kupitia tawi lake la ujumi inachunguza thamani au uzuri wa kitu, ambayo huamua ladha ya kisanii, utamaduni na asili. Pia tawi la maadili huchunguza haki na batili (kipi sawa na kipi sio sawa) kwa jamii. Tawi hili hushughulika na utambuzi wa uzuri na ubaya na huchunguza vyanzo vya asili vya urembo na vile visivyo vya asili vinavyopamba kitu ili kionekane kuwa kizuri katika matumizi, na jinsi watu wanavyofanya uamuzi kuhusu vyanzo hivyo. Msingi ya Nadharia ya Aksiolojia

a) Fasihi huamuliwa kwa uzuri wake wa asili bila ya kuathiriwa na mhemko Msingi huu umetumika katika uchambuzi wa tasnifu hii sababu uzuri wa asili wa filamu unapatikana kwa jinsi filamu inavyowasilisha ujumbe wa kimaadili kwa njia ya kuvutia na ya kimaumbile. Filamu inathaminiwa sio tu kwa maudhui yake, lakini pia kwa jinsi inavyoeleza hadithi, jinsi inavyotumia picha, mwanga, na muziki ili kuunda tajriba ya kuvutia kwa watazamaji. Aidha, maadili yaliyomo katika filamu ndio yametazamwa kama uzuri wa filamu yenyewe.
b) Uzuri wa fasihi unaweza kujitokeza katika matumizi ya lugha ya kisanii. Kanuni hii inasisitiza umuhimu wa lugha, taswira, na mtindo katika kujenga tajriba ya kusoma yenye maana na ya kufurahisha. Lugha ya kisanii ni muhimu sana katika filamu, ambapo matumizi ya mazungumzo huchangia katika kuwasilisha maadili. Filamu za kimaadili hutumia lugha ya kisanii si tu kwa ajili ya uzuri wa lugha yenyewe, bali kwa ajili ya kuimarisha ujumbe wa kimaadili na kufikisha maana kubwa zaidi kupitia taswira na mtindo wa mazungumzo.
c) Fasihi inapaswa kuibua mwitikio wa msomaji. Filamu za kimaadili zinalenga kuibua mwitikio wa watazamaji kwa njia ya kuwafanya wafikiri juu ya maadili, tabia nzuri, na masuala muhimu ya kijamii. Mwitikio huu unaweza kuwa katika mfumo wa tafakari ya kina, mabadiliko ya mtazamo, au hata kuchukua hatua fulani kulingana na maudhui ya filamu.
d) Kanuni za maadili ya jamii huamua kile kilicho sawa ndani ya jamii hiyo; Hivyo ikiwa ni kanuni ya maadili ya jamii inasema kwamba kitendo fulani ni sawa, basi kitendo hicho ni sawa, katika jamii hiyo.

4.0 VIPENGELE VINAVYOJENGA THAMANI YA NDANI YA KIFASIHI KATIKA FILAMU TEULE

Katika utafiti wa makala hii, tumebaini kuwapo kwa vipengele kadhaa vinavyojenga thamani ya ndani ya kifasihi. Miongoni mwa vipengele vilivyobainika ni kama vifuatavyo

4.1 Usawiri wa Wahusika Kimajazi

Wahusika wa Kimajazi katika fasihi ni wahusika ambao hutumika kuwakilisha dhana, maadili, au fikra juu ya kile wanachokifanya katika mfumo wa kimajazi. Wahusika hawa hawaonyeshi tu tabia au hali zao binafsi, bali wanakuwa na maana kuhusiana na masuala ya kijamii, kisiasa, kimaadili, au kifalsafa. Wahusika wa kimajazi, mara nyingi, hutumika kutengeneza tafsiri maalumu au kuhamasisha mtindo wa kifasihi. Ndio maana, ni muhimu kuchunguza namna wahusika walivyosawiriwa na namna wanavyochangia uendelezaji wa maana **[9].** Hoja hii inaonesha wahusika wanavyoweza kubebeshwa maana kama ilivyojitokeza katika filamu teule

Tukianza na *Wali Wangu*, wahusika wamepewa majina kwa mujibu wa ishara ya kitabia. Tabia za wahusika hao ndio zinasawiri majina yao. Kwa mfano, mhusika Suruali na Shata wanapewa tabia ya uzinzi. Suruali ni vazi lenye miguu miwili linalovaliwa toka chini hadi kiunoni **[1].** Katika jamii ya

Waswahili, suruali ni vazi linalonasibishwa na wanaume. Pia, jamii ya Waswahili wa Pwani imekuwa ikitumia jina la 'mwanamme suruali' kumaanisha mwanamme asiyekuwa na pesa ila anapenda sana wanawake katika masuala ya ngono.

Shata ni masalio yanayobaki baada ya tuwi la nazi kuchemshwa na kugeuka mafuta **[1].** Jamii ya Waswahili hutumia neno 'shata' kumaanisha mtu anayejivuna na kujiona kuwa anavutia katika uga wa mapenzi, hasa kwa mwanamke. Neno hili hutumika sambamba na neno 'mafuta'. Hutumika kwa kusema mwanamke fulani ana Shata au ana mafuta. Pia, katika baadhi ya muktadha wa kijamii, 'shata' hutumika kama sehemu ya mitindo ya mavazi inayoweza kuhusishwa na tabia za kijinsia zisizokubalika au zinazoshabihiana na uzinzi. Hii ilianza wakati wa mabadiliko na ushawishi wa mitindo ya mavazi kutoka kwa tamaduni za nje ambazo zilikubalika katika miji lakini ziliangaliwa kwa mtazamo wa kifamilia au kimila kama zisizofaa. Kwa ujumla, majina ya Suruali na Shata yametumika kama ishara zinazoenda sambamba na tabia za wahusika waliopewa majina hayo. Maelezo hayo yanathibitishwa na matendo ya wahusika hao. Wahusika hawa kila wanapokutana huona ndio fursa ya kufanya uzinzi. Ithibati ya tabia hiyo imo katika dayalojia ifuatayo:

Shata: Kwani una haraka ya nini?
Suruali: Sio haraka, bali tukishiriki tendo itaweza kutudhibitishia kuwa sisi ni wapenzi, na mimi nitapata fursa ya kukusifu kwa kila tamu.
Shata: Ndiyo maana nikakwambia kesho ntakuwa nshajiandaa kwa jambo hilo.
Suruali: Si dhani kama kujiandaa itajenga usahihi wa kushiriki ipasavyo. Naomba nikutumie leo na kesho ntakutumia tena, sitaki kupoteza fursa hii sehemu tuliyopo….
Chanzo: *Wali Wangu*, onesho la 1, dakika ya 10:14 hadi 11:00

Eneo jingine linaloonesha Shata na Suruali ni wapenda ngono kupitiliza ni pale Shata anapotoroka kwao na kukimbilia kwa mwanaume. Shata anatoroka na kulala kwa Suruali ili kupata fursa ya kufanya ngono. Aidha, katika filamu hii tunaoneshwa maeneo mengi yanayohusisha ngono. Kwa mfano, Mama Shata anaranda mitaani kutafuta mwanawe wanakutana na Fidodido na mazungumzo yao yanakuwa hivi:

Fido Dido: Kulikoni naona unataka kujikwaa na kuongea peke yako?
Mama Shata: Namtafuta Shata.
Fido Dido: Mwanao ameshauonja utamu wa muhogo, nadhani hatarudi tena kunyonya maziwa, aah, subutu.
Chanzo: *Wali Wangu*, onesho la tatu, dakika ya 00:07 hadi 00:29)

Maelezo ya Fido Dido yasemayo "mwanao ameshauonja utamu wa muhogo, nadhani hatarudi tena kunyonya maziwa, aah, subutu" yanaashiria kuwa Shata ameshakuwa mzoefu katika kufanya tendo la ngono. Hivyo usawiri wa majina yao ndio unaonesha kuvishwa kwa uhusika wa namna hii. Jambo hilo linathibitishwa na kutiliwa mkazo na mmoja wa waigizaji na mtunzi wa filamu ya *Wali Wangu* wakati akihojiwa na chaneli ya studio 9 entertaiment, pale aliposema:

> *Shata ni neno linalotumika katika muktadha wa mavazi. Kwa kawaida, Shata ni Suruali ndefu au nguo za aina fulani, lakini katika jamii ya Waswahili, linapotumika katika muktadha wa tabia za kijinsia humaanisha mtu anayependa ngono. Pia, linaweza kumaanisha mavazi au mitindo ya kijinsia isiyo na maadili*.[1]

Nukuu hii inaonesha mitindo ya uvaaji isiyokubalika katika jamii ya mtunzi wa filamu hii. Pia, neno hili linaonekana kama msimu tarafa, ambao jamii ya mtunzi wa filamu huutumia kama jina na mtu anayependa ngono. Hivyo majina hayo (Suruali na Shata) ni majina ya kimajazi yenye maana ya mtu anayependa ngono. Kwa jumla utumiaji wa majina haya yamejenga thamani ya kazi hii ya fasihi, kama inavyoelezwa katika msingi wa Aksiolojia unaeleza kuwa thamani ya kazi ya fasihi inaweza kujitokeza katika matumizi ya lugha ya kisanii, taswira, na usawari mzuri wa wahusika katika kujenga kazi yenye maana na ya kufurahisha. Hivyo, jina la Shata na Suruali limechukua ni ishara inayotokana inayoendana na miktadha ya jamii na kukubali kuwa majina hayo yanasibiwa na matendo ya wahusika.

Majina mengine yanayodokeza ishara fulani katika kazi hii ya kisanaa ni pamoja na Chujio, Katambuga, Sulupu. Pia, majina haya yanadokeza Uafrika ndani yake. Majina kama Chujio, Katambuga, na Sulupu ni mifano mizuri ya majina ya Kibantu ambayo yanadokeza ishara fulani na kutoa maana na uhusiano mkubwa na tamaduni za Kiafrika lakini msingi mkubwa ni kusisitiza kuwa jamii ya Waswahili nayo ina majina yake.

Pia, mhusika Mwalimu ni miongoni mwa majina ya Kiafrika yanayoitwa kwa kulenga mtu kuwa na hekma na maarifa katika jamii. Ujuzi na maarifa na matendo ya Mwalimu yanathibitisha kweli kuwa huyu ni mwalimu kutokana na hekima pamoja na maarifa aliyonayo. Katika filamu hii, mwalimu anatumiwa kama kiungo cha utatuzi wa matatizo ya jamii. Kila mtu anaonekana kurejelea hekima ya mhusika huyo, aidha, mhusika huyu anaandaa mafunzo kwa wanafunzi wake ili kuwapa maarifa ya ukombozi wa jinsia na kujielewa. Haya tunaoneshwa katika mazungumzo yafuatayo:

Mwalimu: (*anawaimbisha nyimbo wanawake waliohudhuria mkutano*)
japo kwa kuchachenieleze, nieleze wali waangu x2

Wali: (*wanaitikia*) japo kwa kuchache tueleze, tueleze
wali wako x2

Mwalimu: Kitanda cha wanandoa ndio sehemu pekee cha kupatanisha migogoro inayotokea …

Chanzo *Wali Wangu* onesho la 2, dakika 43: 19 hadi 46:54

Kusanyiko la darasa linajitokeza katika maonesho yote ya filamu ya *Wali Wangu*. Kwa mfano, onesho la 1, kuazia dakika 7:57 ya hadi 12:49, onesho la 2, kuanzia dakika ya 8:27 hadi, na onesho la 5, kuanzia dakika 4:20 hadi 5:58. Jina la walimu katika filamu ya *Wali Wangu* linaonyesha uhusiano mkubwa na dhana za Uswahili na ubantu. Katika tamaduni za Kiafrika, hasa katika jamii za

[1]Mahojiano ya nje ya pazia (*behind the scene*) yaliyofanywa baina ya Madebe Lidai, muigizaji wa filamu ambaye pia ni mtunzi wa filamu ya *Wali Wangu* na mwandishi Faqueen Guga wa chaneli ya mtandaoni ya *Youtube* ya studio 9 entertaiment.

Kiswahili, walimu hawakuwa tu watu wa kufundisha masomo, bali pia walikuwa viongozi wa kijamii, waliokuwa na jukumu la kuleta mabadiliko katika jamii zao.

Katika filamu hii, mwalimu anachorwa ni mtu wenye dhamira ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu maadili, haki na umoja. Kwa hivyo, jina "mwalimu" linavuma kwa maana ya kuwa mtu anayechochea mabadiliko, anayejali ustawi wa jamii na ambaye ana uhusiano wa karibu na watu.

Pia, walimu anafanikiwa kuiteka jamii kwa taaluma yake na maarifa aliyonayo. Walimu katika filamu hii anachorwa kama mhusika muhimu katika mchakato wa kijamii na wa kielimu, na yanawakilisha mifumo ya ushirikiano, usawa na mabadiliko katika jamii. Hali hiyo inaonekana kwa mhusika huyo kila anapoweka vikao vya madarasa yake. Mfano mmojawapo ni pale aliposema:

Batani:	Siku hizi hapa kijijni asilimia kubwa na wasichana wamekuwa wanyenyekevu na kubadilika tabia, hili darasa kama lingeanza zamani lingesaidia.
Mke wa Batani:	Mwalimu kasema kuna vitu wengine vya ukoo huwa havibadiliki
Batani:	Ina maana hii asilima chache iliyobadilika ni tabia
Mke wa Batani:	Ndio mwalimu ametusaidia kutambua jinsia yetu
Batani:	Basi ndio mmshukuru huyo mwalimu wenu.
	Chanzo: *Wali Wangu*, onesho la 3, dakika ya 27:27 hadi 27:52)

Katika mazungumzo hayo, tunapata picha ya wazi ya jinsi mwalimu anavyofanikiwa katika kusibu jina lake, kwa maana kwamba amefanikiwa kutimiza jukumu lake la kuwafundisha na kuwapa wanawake ufahamu kuhusu nafasi zao katika jamii. Hapa, mke wa Batani anasema kwamba mwalimu amewasaidia kutambua jinsia zao, jambo ambalo lina maana kubwa katika muktadha wa maisha ya kijamii.

Kwa upande wa filamu ya *Matusi*, majina ya kimajazi yametumika ili kuibua dhamira zilizokusudiwa. Mhusika Kutafuna na Chanuo Nchakali ni miongoni mwa majina yaliyotumika kwa kuzingatia ishara ili kutoa dhamira fulani. Kwa mfano, Kutafuna jina hili linatokana na neno tafuna. Tafuna ni kitendo cha kukatakata au kubana chakula au kitu chingine kwa mfano **[1]** Kutafuna amechorwa kuwa mhusika mwenye maneno makali na yenye kuchoma. Kutafuna anamtafuna kila mtu kutokana na maneno yenye matusi na kejeli. Ithibati ya hoja hii tunaoneshwa katika mazungumzo yafuatayo:

Kutafuna:	Samahani mkwe, hicho ulichovaa ni nini?
Chanuo:	Nilichovaa wapi?
Kutafuna:	Kichwani.
Chanuo:	Ni urembo.
Kutafuna:	Na hiyo mikucha kuwa mirefu… kwa iyo mjomba ndio. umependa mwaamke wa aina hii ...

Chanzo: *Matusi* onesho la 1, dakika ya 8:33 hadi 9:25

Jina la Katafuna ni ishara. Ishara hii inaonesha namna anavyowatafuna wahusika wengine kwa kuwaweka wazi maovu yao pamoja na matendo yao yanayovunja maadili katika jamii. Mfano, katika

mazungumzo haya, jina la Kutafuna linaibua matumizi ya lugha yenye kuonesho ukali wa maneno. Kutafuna anatumia maneno yenye ukali na dhihaka, huku akimkejeli Chanuo kwa kuvaa vitu vinavyoonekana kinyume na muktadha wa kijamii. Ifahamike ya kwamba kumuelekeza mtu sio tatizo bali namna ya kuelekezaji ndio umeibua tatizo.

Kutafuna anatumia dhihaka na bila kujali kuwa mgeni huyo ndio siku ya kwanza kuja kijiji hapo. Swali la Kutafuna liulizalo “hicho ulichovaa ni nini" linaonyesha kutokubali au kutofurahishwa na kile anachovaa Chanuo. Hii ni kwa sababu Nadharia ya Aksiolojia, kupitia tawi la maadili, inazungumzia msingi wa kukubaliwa au kukataliwa kwa matendo na jamii ni miongoni mwa maadili ya Waswahili.

Pia, Kutafuna anaendelea kuuliza "Na hiyo mikucha kuwa mirefu … kwa iyo mjomba ndio umependa mwanamke wa aina hii …" Hapa, Kutafuna anacheka au kudhihaki kuhusu jinsi Chanuo alivyobuni muonekano wake kwa kutumia mikucha mirefu.

Kwa upande wa mhusika Chanuo Nchakali, Jina lake linatoa taswira ya nguvu, changamoto, na upinzani. Kila neno katika jina hili linaweza kuleta maana maalumu. Chanuo ni kifaa kinachotumiwa na wanawake katika kusuka nywele. Kifaa hicho ni lazima kiwe vijiti vilivyosimama na kuwa na ncha. Mtunzi akaamua kufafanua kwamba ncha hizo ni kali kwa sababu zinaweza kumchoma kila mtu hata kama hana hatia. Hali hiyo ya kuchoma imejitokeza kwa mhusika huyu kuwa na ufedhuli na maneno machafu, mkosefu wa adabu na haheshimu hata wakubwa zake. Kusawiri kwa jina hilo kumembebesha mhusika huyo tabia hizo. Mazungumzo yafuatayo ni mfano wa maeneo aliyotovuka adabu ni:

Chanuo: Huku kijijini kwenu kuna wanaume wachafu. (*Anatema mate mbele ya mtu mzima*)

Bashite: Huku ndiko alikozaliwa marehemu mama yangu. Hii hali wenyewe wameshaizowea, yaani wamezoweana

Chanuo: Ningekuwa naishi huku kila siku ningekuwa natapika (*anafinya pua na mdomo*)

Chanzo: *Matusi,* onesho la 01, dakika 5:42 hadi 6:08

Pia, Kambaulaya, Bashite, na Batani ni mifano ya majina halisi ya Kiafrika ambayo mtunzi wa filamu hii ameyatumia ili kuzifanya filamu zake kuwa bora na kuwa na uhalisi wa Mswahili. Hii ni kinyume na watunzi wengi kama anavyosema **[5]** ambaye anabainisha kuwa watunzi wa filamu za Bongo wanavyoathiriwa na Unaigeria hadi kwenye majina ya wahusika na majina ya filamu zao. Anabainisha kuwa filamu nyingi za Kanumba zimeitwa kwa majina ya kiingereza. Kwa mfano, *Dar to Lagos* (2006), *She is my sister* (2006), *The director* (2006) na *Penina Jezebel’s Daughter*.

Uamuzi wa mtunzi kuita filamu zake *Wali Wangu* au *Matusi* pamoja na kuita wahusika wa filamu hizo kwa majina ya Kimajazi unaendana na fikra za Nadharia za Aksiolojia yenye lengo la utambulisho wa thamani ya mswahili. Hii ni kwa sababu nadharia hii inaangazia jinsi majina, alama, na mifumo ya kijamii inavyotumika kuthamini kitu kwa uzuri wake.

Batani, Shata Shuruali, Katambuga, Chujio, Mwahija, na Sulupu ni baadhi ya majina ya wahusika wanaotumika katika filamu za utamaduni wa Kiswahili.

Hivyo, majina ya wahusika sio hupachikwa tu bali hutakiwa yawe na maana kwa mujibu wa jamii inayofikishiwa kazi hizo. **[10]** anasema waandishi huteua majina ya wahusika wao na kufungamanisha na matukio kwa lengo la kudokeza maana kwa hadhira. Ufafanuzi wa ufunganishaji wa matukio ndio unaonesha kuwa majina huwa yana ishara na maana mahususi. Pia, wahusika hutumika kudokeza falsafa ya mwandishi na ya jamii kwa jumla. Kwa msingi huu, ndiyo maana kazi ya Matusi na Wali Wangu zinawasilisha falsafa iliyofumbatwa katika jadi za Waswahili.

4.2 Mbinu ya Utomeleaji

Utomeleaji ni mbinu muhimu katika kuonesha na kuwasilisha thamani ya ndani ya kifasihi. Hii ni kwa sababu utomeleaji unahusisha jinsi ambavyo mtaalamu wa kifasihi anavyoelezea na kuwasilisha mambo ya kifasihi kwa njia inayovutia, yenye maana na yenye kuonyesha ufanisi wa kipekee wa kazi fulani ya kifasihi. **[12]** anasema kuwa utomeleaji ni mbinu inayohusiana na kuchopeka vipande vya utanzu mwingine ulio tofauti na utanzu unaoshughulikiwa. Hapa anaonesha kuwa utanzu unaoshughulikia unaweza kuwa riwaya lakini ndani kuna ushairi, au tamthilia lakini ndani yake kuna barua au kinyume chake. Hivyo, msanii hawezi kumudu mbinu hii kama sio mbunifu mzuri wa kazi ya fasihi.

Utomeleaji ni dhana inayotumika katika kuifanya kazi ya fasihi iwe bora kwa kuchopeka mbinu na mitindo tofauti kwenye kazi ya sanaa. Katika filamu ya *Wali Wangu* na *Matusi*, utomeleaji umekuwa kipengele muhimu kinachojenga usanifu wa kazi ya filamu hizi.

Tukianza na filamu ya *Matusi*, mtunzi amechopeka nyimbo ndani ya filamu. Uchopekaji huu wa nyimbo haukufanywa kwa bahati mbaya bali ulidhamiriwa katika kubeba tukio la msingi. Hali hii ya filamu za kileo kutumia nyimbo za jadi na kutumbuiza kwa ngoma za asili ni ubunifu wa hali ya juu kwa sababu sio kawaida. Ubunifu huu unaturudisha kwenye Sanaa za maonesho au tamthilia za jadi. Mtunzi wa filamu anaanza na midundo ya ngoma wakati filamu ikiwa inaanza kwa kila onesho. Midundo ambayo huwa inatoa ishara ya dhamira itakayozungumziwa eneo hilo. Mbali na midundo hiyo uchopekaji wa nyimbo za asili zinajitokeza katika kila tukio. Kwa mfano, sehemu zote zinazoonesha umuhimu wa jadi za Kiafrika, mtunzi wa filamu ameweka wimbo ufuatao:

> *Mwanangu kua uyaone ya dunia ilipofikia na inapoelekeax3*
> *Tusiyaone mughali yetu tukayagumika*
> *Tunazo kila dalili kumbukumbu kuziweka*
> *Karabai na kandili vifaa vilitumika umeme wa kitajiri ndio ulofahamika*
> *Matusi,* Onesho la kwanza dakika ya 17: 03 hadi 18: 16

Pia, utomeleaji wa wimbo umetumika wakati mtunzi akionesha utovu wa adabu unaofanywa na wahusika wake. Wimbo huu umetumika kama kipengele maalumu cha kisanaa ambacho kinajenga thamani ya kazi hiyo. Kipengele hiki kimekuwa kinaifanya kazi hii kuwa na mvuto wa kipekee wa kisanaa kwa namna wimbo huo unavyoimbwa na unavyoendana na kinachozungumzwa katika kitendo husika. Mishororo yake ni hii ifuatayo:

Matusi hayo, ooh Matusi hayo, Matusi hayo.
Wee mwana Matusi hayo
Kwenda uchi ukweni, Matusi hayo
Kutopita jandoni, Matusi hayo
Mchezo wa wawatoto kuchezwa na wakubwa, Matusi hayo.

Wimbo mwingine umejitokeza kwenye onesho la 1, dakika ya 15: 32 hadi 15:59. Mishororo yake ni hii ifuatayo:

Wanawake wa kileo aaaah
Wajiona ndio wao, ooooh
Wanawake wa mjini wameacha asili zetu
Waendekeza uhuni kufuata mila za watu, aah wanawake wa kileoo
Wameacha mila zao, aaah x3

Chanzo: *Matusi,* Onesho la 1, dakika ya 15: 32 hadi 15:59

Kupitia utomeleaji wa nyimbo, mtunzi wa filamu hii anaonesha dhamira ya mabadiliko ya kijamii na utamaduni ambayo yanahusiana na wanawake wa kisasa, hasa wale wa mijini, na athari za kuiga tamaduni za kigeni kwa kupuuza mila na desturi za asili za jamii zao. Wimbo unaelezea hali ya wasiwasi kuhusu jinsi wanawake wa kileo wanavyojiona kuwa bora au wa kisasa zaidi kuliko wanawake wa zamani, lakini kwa njia ambayo inahatarisha utamaduni wa kiasili na kuleta mabadiliko yasiyohitajika. Mtindo huu umeijengea thamani kazi hii kutokana na kuipamba kisanaa. Wimbo ni kipengele kinachotumika kujenga mvuto wa kisanaa kwa kazi ya kifasihi. Maelezo hayo yanathibitishwa kupitia msingi wa Nadharia ya Aksiolojia inayoeleza kuwa uzuri wa fasihi unaweza kujitokeza katika matumizi ya mbinu mbalimbali za kisanaa.

Mtindo wa ngonjera nao umejitokeza kama mbinu ya kuthaminisha filamu hii. Sehemu zilizotumika mtindo wa ngonjera ni zile zilizodokeza kibwagizo na kukifanyia uradidi mara kwa mara. Ufuatao ni mfano wa mtindo wa ngonjera katika filamu ya matusi:

Kutafuna: *Huyo mwanamke wako anatakiwa akuheshimu na sio kukuogopa; na heshima haiji wa magumi hebu niachie mimi nguruwe nimfunde mwari wako. Niachie mimi nguruwe nimfunde mwari wako x3*

Chanzo*: matusi Onesho* la 1, dakika ya 23: 18 hadi 23: 38

Pia mtindo huu umejitokeza tena katika onesho la 1, dakika ya 24:17 pale mjomba (Kutafuna) anaposisitiza kuwa kipigo hakiwezi kufanya mwanamke awe na adabu. Kutafuna nasema:

Kutafuna: *Mjomba, tatizo lako wewe ni moja tu, umetahiriwa hospitali, hujayaona maumivu wakati ulipopigwa sindano na kukatwa govi, wewe mjomba ghariba wako ni mwanamke. Niachie mimi nguruwe niwe Ngariba wake. x2*
Acha na ye awe na Ngariba wake x3

Chanzo: *Matusi,* onesho la 1, dakika ya 23: 17 hadi 24: 27

Kurejea rejea kwa kibwagizo au kiitikio cha maneno ni mtindo uliotamalaki kwenye ngonjera hasa za majukwaani. Mtuzi wa filamu hii ametomelea mtindo huu na kuonesha uasili wa sanaa zetu za

maonesho na upya wa mitindo wa filamu. Hii ni kwa sababu watunzi wa filamu za Bongo wameacha tamaduni hii na kuanza kuiga sanaa za mataifa mengine.

Kwa upande wa filamu ya *Wali Wangu*, utomeleaji wa nyimbo umetumika katika kila mwanzo wa onesho la filamu hii. Katika maonesho yote, wimbo ulitumika ili kutoa dhamira mahususi kwa jamii. Pia, mtunzi wa filamu hii anavuka mipaka ya kutumia utomeleaji wa nyimbo zake za jadi tu, bali anachopeka wimbo wa Marijani Rajabu kupitia redioni. Ufuatao ni sehemu ya wimbo huo:

Niulizieni enyi walimwengu
Huyu mwanamme anavyonitesa
Hii ndio haki au nimateso x2
Kanitoa kwetu kwa baba na mama
Kwa vigelegele na heshima nyingi
Chanzo: *Wali Wangu*, onesho la 1, dakika ya 23: 43 hadi 24:06, wimbo wa Marijani Rajab

Wimbo huu unabeba dhamira ya kudokeza majukumu ya mume wakati Fidodido anakatazwa kuwatesa wanawake pale atakapoingia katika ndoa. Filamu ya *Wali Wangu* inalenga kuonesha namna wanandoa wanavyopaswa kuwajibika katika ndoa zao. Hivyo, kudokezwa kwa wimbo huu kwenye filamu ulilenga kuzungumzia wasichana wanavyopitia maumivu na mateso kutoka kwa mpenzi. Wimbo unamchora msidhana dhalili anayeomba msaada na kueleza hali yake kwa dunia, akionyesha jinsi anavyoteseka kutokana na mapenzi.

Wimbo mwingine ni ule unaojitokeza kila mwanzo wa onesho la filamu hii. Kwa vile filamu ililenga kufundisha desturi za kijamii hasa za ndoa. Wanawake au wari walikumbushwa kila mara filamu ilipoingia kwenye onesho moja Kwenda jingine. Utomeleaji huo ulikuwa na lengo la kuwafundishwa wanawake namna ya kuwajibika. Wimbo huo unasema:

Wali Wangu naomba tusikilizane,
Wali Wangu, ukweli tuambiane
Maneno yenye tija uyaweke kichwani,
Omba ruhusu chuja, uyatilie akilini
Ndoa ni mali yako
Baraka ya muumba wako
Ikikutoka mikononi mwako
Huo ni ujinga wako, kisavu usitike karanga,
Ukawapende maadui zako.
Chanzo: *Wali Wangu*, onesho la 1 dakika ya 6:43 hadi 8: 06

Wimbo huu unaafikiana na Nadharia ya Aksiolojia kupitia tawi la maadili. Hii ni kwa sababu unatoa ujumbe wa maadili kuhusu uhusiano wa ndoa, familia, na heshima kwa mume/mke. Wimbo huu umejaa mifano ya maadili ambayo inasisitizwa juu ya umuhimu wa uaminifu, upendo, na kuheshimu ndoa. Kupitia nadharia ya maadili, tunaweza kuelewa maana ya wimbo huu. Wimbo unasisitiza adili muhimu ya kwamba kabla ya kuchukua hatua yoyote muhimu katika ndoa au uhusiano, mtu

anapaswa kufikiri kwa umakini na kuchuja mawazo yake kwa hekima. Kufanya hivyo kunaepusha kufanya makosa ambayo yanaweza kuharibu uhusiano.

Utomeleaji mwingine unaojitokeza katika *Wali Wangu* ni usimulizi wa hadithi ndani ya filamu hiyo. Usimulizi huu umetokana na ufundi alionao mwandishi katika kuichombeza filamu yake. Hadithi inayosimuliwa ndani ya filamu hii inadhamiria kujenga na kuendeleza dhamira zilizotumika. Hadithi hii inaibuka baada ya mwalimu kuulizwa swali na Batani. Swali hilo ni: "Kwa nini mwalimu unataka tuwe wanyeyekevu kwenye kila jambo?" Yafuatayo ni majibu ya Mwalimu:

> ***Mwalimu**: Siku moja simu ya muumini iliita kwa bahati mbaya katika nyumba ya ibada. Kiongozi wa ibada alitoa karipio na kumuonesha muumini huyo ni miongoni mwa waumini wazembe. Baada ya ibada waumini wengine waliendelea kulaumu kwa kusababishiwa usumbufu katika ibada yao. Mkewe naye hakubaki nyuma, aliporudi nyumbani akaendelea kumlaumu kwa uzembe wake, ndugu wengine nao walitikisa vichwa kuonesha kutoridhika na tukio lile … yule jamaa aliendelea kufedheheka na kuaibika. Jioni ile aliona bora akanywe pombe huko kilabuni, kwa vile hakuwa mzoefu alimwaga kinywaji chake kwa bahati mbaya na kuwamwagikia baadhi ya walevi. Wale waliomwagikiwa na kinywaji chake walimkimbilia, ghafla alifumba macho kwa kuhofia kuwa atazabwa vibao au kuambiwa maneno makali. Lakini walimsongelea hadi sikioni na kumuuliza vipi hujaumizwa na vipande vya chupa vilivyovunjika? Akaja mhudumu na kumpa kitambaa ajisafishe. Ghafla mwanadada kiongozi wa kilabu kile alikwenda na kumpa bia nyingine kufidia bia iliyomwagika huku akimpiga busu na kumwambia usihofu hakuna aliyekamilika. Basi hadi hapa tunapoongea yule jamaa hajaacha kwenda kilabuni.*
>
> **Chanzo**: *Wali Wangu*, onesho la tatu, dakika ya 13:14 hadi 15:11

Nukuu hii inaonesha kuwapo kwa hadithi ndani ya hadithi ni ustadi mkubwa wa kuonesha dhamira zilizomo. Hali hii inatokana na ujuzi na ufundi wa mtunzi wa kutambua thamani ya Fasihi kwa sababu fasihi hii ni ya Waswahili. Hivyo, ametumia mtindo uliopo kwenye fasihi simulizi ya Kiswahili, jambo ambalo ni nadra sana kwa watunzi wa filamu wa kileo.

Utomeleaji huo umebeba taswira nzima ya lengo la filamu hizo. Ingawa watunzi wengi wa filamu wanadhani utanzu mmoja una uwezo wa kujitegemea na kusimama peke yake, hali hiyo sio kweli na haileti kazi yenye ubora. Kwa msingi huo, filamu ya *Wali Wangu* na *Matusi* zimebeba thamani ya kifasihi kutokana namtindo wake wa matumizi ya mbinu ya utomeleaji katika filamu hizo. Hivyo thamani ya kifasihi katika filamu hizi imestawi barabara.

4.3 Mbinu ya Utenguzi

Neno utenguzi linatokana na kitenzi "tengua" kinachozaliwa kutokana na mnyambuliko wa kitenzi "tenga" katika kauli ya kutendua. Kitenzi hiki kinaunda kitenzi "tengua". Kutengua ni hali ya kukiondosha kitu kutoka katika nafasi yake ya awali ili kitu kingine kiweze kuchukua nafasi yake,

[17] Katika fasihi, utenguo unaweza kudhihirika kwa namna tatu kuu: utenguano wa ndani ya mfumo, utenguano wa kiwakati au kihistoria na utenguo wa tanzu kwa tanzu. Utenguo wa kimfumo ni ule ambao tanzu tofauti hugombania nafasi ndani ya mfumo mmoja kwa kufyatuana. Kwa mfano, utanzu mmoja unaweza kubebwa na utanzu mwingine. Utanzu huo uliojiingiza ndani ukawa unakamilisha dhima ya kile kilichokusudiwa. Mtenguo wa kihistoria ni ule ambao tanzu zinazofanana au kutofautiana zinatenguana ndani ya mfumo mmoja kwa mujibu wa mpito wa wakati.

Katika utafiti wa makala hii, tumebaini kuwapo kwa mtenguano wa kimaelezo (tanzu kwa tanzu) [15] anasema, utenguo wa tanzu kwa tanzu unahusisha tanzu za aina moja kufyatuana na kushindania nafasi moja. Kwa mfano, methali moja inaweza kuitegua methali nyingine, au maelezo fulani yanaweza kuyategua maelezo mengine na kuleta maana. Mara nyingi, utenguzi huwa unajitokeza kwa sura ya kupingana kwa muonekano wa nje lakini kukubaliana kwa muonekano wa ndani.

Katika filamu ya *Matusi*, utenguzi wa kimaelezo umejitokezakwenye maeneo mengi kama mbinu ya kiufundi ya mtuzi. Miongoni mwa maeneo yaliyotokea utenguzi ni onesho la kwanza. Kama inavyosomeka:

Kutafuna… Heshima haiwezi kuja kwa magumi, siku zote nakwambia usimpige mwanamke.
Bashite: Sasa mimi kosa langu lipi hapo. Eeh, Kumkataza kitu ambacho hakihitajiki?
Kutafuna: Kosa lako ni moja tu.
Bashite: lipi? Eeh.
Kutafuna: Kosa lako mjomba, wewe umetahiriwa hospitali. Hukupata maumivu wakati ukikatwa govi, wewe gariba wako mwanamke mjomba, sasa muwache naye apate ngariba wake kabla ya wewe kumuoa.

Chanzo: *Matusi* onesho la 1, dakika 23: 23 hadi 24:14

Nukuu hii inaonesha maneno ya Kutafuna yanayotengua maneno ya Bashite. Kwa mfano, kauli isemayo "Kosa lako ni moja tu" pamoja na "Wewe umetahiriwa hospitali. Hukupata maumivu wakati ukikatwa govi, wewe ngariba wako mwanamke mjomba, sasa muwache naye apate ngariba wake kabla ya wewe kumuoa." Jibu la Kutafuna linahusisha suala la kutahiriwa na maumivu ya wanawake, lakini halina uhusiano wa moja kwa moja na suala la heshima kwa wanawake au kupiga wanawake, ambayo ndiyo mada ya awali. Utumiaji huu wa lugha umekuwa wa kisanaa sana kiasi cha kuijengea mvuto kazi hii na hivyo kuonekana kuwa na thamani ya kifasihi kwa mtazamaji.

Hata hivyo, utenguaji huu unalenga kitu kile kile kwa maana ya ndani. Kauli ya Kutafuna inajibu swala la msingi la Bashite. Kutafuna anaanza kwa kusema, "Heshima haiwezi kuja kwa magumi, siku zote nakwambia usimpige mwanamke." Hii ni kauli ya kupinga vurugu dhidi ya wanawake na inazungumzia umuhimu wa heshima kwa wanaume waliokwenda jandoni. Kwa mujibu wa misingi ya jando, ngariba ni mtu anayepaswa kuheshimiwa sana. Hivyo kutafuna akimpiga mwanamke anampiga ngariba wake, jambo ambalo ni utovu wa nidhamu. Pia, wanaume waliokwenda jandoni wanafundishwa namna ya kukabiliana na changamoto za ndoa na utatuzi wake. Hivyo, wanaume aliyepata mafunzo ya jando ni mwiko kumpiga mwanamke.

Utenguano mwingine unajitokeza kwa maneno ya kutafuna pale anapomkanya chanua kuhusu tabia zake mbaya. Maelezo ya kutafuna yanajitokeza hivi:

> **Kutafuna:** *...Na mlivyokosa maarifa mnapenda sana pesa kuliko tendo lakini mnapata sana mimba kuliko utajiri. Jambo ambalo linawafanya muwe watowaji wazuri wa mimba kuliko sadaka*

Nukuu hii inaonesha namna maelezo ya Kutafuna yanavyotenguana. Utenguzi huo unakosa mantiki na maana kwa sababu unachanganya mawazo yasiyoendana. Kutafuna anatoa kauli ambazo hazina muktadha wa moja kwa moja na zinazojenga upinzani kati ya dhana za pesa, mimba, sadaka, na tendo la ndoa. Hii inafanya mazungumzo kuwa ya kuchanganya na yasiyo na muunganiko mzuri, na hivyo kupingana kimantiki na kimaana.

Maelezo ya Kutafuna yanapita katika maoni tofauti bila kutoa muktadha wa wazi. Anasema kuwa watu wanapenda pesa kuliko tendo la ndoa na wanapata mimba nyingi, lakini baadaye anasema wanakuwa "watoaji wazuri wa mimba kuliko sadaka." Hii ni kauli isiyo na muktadha wa kimaana. Hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kupenda pesa na kutokuwa na sadaka, au kupata mimba na utoaji wa mimba. Katika kutoa mafundisho ndiko yanapokutana maelezo hayo kwa kukutanisha tabia za wanawake.

[15] alifafanua kuhusu amesema, utenguzi wa maana huwa hauoneshi maana ya wazi, maana zake huwa zinafichwa kutokana na kutoana kimantiki na kimaana kwa maelezo au kwa utanzu. Mara nyingi mtenguano huu huwa unazifanya fasihi ziwe ngumu kufasiri. Lakini ziwe nzuri kutokana na ufundi wa kucheza na maneno.

4.4 Usawiri wa Mandhari

Usawiri mzuri wa mandhari ni kipengele kimojawapo kinachoonesha kithamani katika filamu. Filamu hutathiminiwa kutokana na sehemu ambayo filamu hiyo imeigizwa. Jukwaa au sehemu ya kuchezea filamu hutegemewa kuwa na mvuto wa aina yake. Katika ujenzi wa mandhari ya filamu huzingatiwa dhamira, wakati na walengwa. Vipengele hivyo vinaungwa mkono na **[13]** alipoeleza kuwa mandhari hujumuisha wakati, mahali na muktadha ambamo kazi ya fasihi inatendwa. Naye, **[7]** na **[18]** wanaona kuwa vipengele vikuu vinavyojenga mandhari ni mahali na muktadha wa kazi husika. Maelezo ya wataalamu hao yanaenda sambamba na ripoti hii ya utafiti. Kwa sababu katika filamu ya *Matusi* na *Wali Wangu* yamebainika mandhari katika vipenge viwili. Nazo ni muktadha na dhamira.

Kupitia filamu ya *Matusi* na *Wali Wangu*, muktadha wa mandhari ulilenga sehemu itakayotoa taswira ya jadi na utamaduni halisi wa Mswahili. Jadi hizo lilioneshwa kupitia majengo na makazi. Mtunzi wa filamu hizi anaonesha hali iliyopo katika vijiji vya Tanzania kuwa na makazi duni. Katika maonesho yote nyumba za makazi zinaonekana kwa duni (nyumba za tope).

Kwa upande wa huduma za jamii zinaonekana kuwa duni. Kwa mfano, maji yanayotumika kwa ajili ya matumizi sio safi wala salama. Katika onesho la kwanza katika filamu ya *Wali Wangu* wanaonekana wanawake wakielekea bondeni kuchota maji. Pia, onesho la 4, dakika ya 3:49 hadi 4: 05 wanakijiji wanaonekana kwenye shimo la maji wakiwa wanachota maji kwa ajili ya matumizi ya

kila siku. Pia, katika *Matusi* wanawake wanasaka maji kwenye panga, mashimo na visima vya jadi. Hali hii bado inaonekana ni tatizo linaloikabili jamii katika huduma za jamii. Mtunzi wa filamu hii ameamua kutumia mandhari hayo ili kuonesha thamani ya fasihi ya Waswahili kwa sababu inachora mandhari halisi ya Waswahili hao. Ushahidi wa hili unaoneshwa pale wanakijiji walipokusanyika katika shimo na kuanza kuchota maji kwa ajili ya matumizi.

Chanuo: Huku ndio mnakuja kuchota maji, sasa maji haya ndio tunayatumia, si na wanyama wanakuja kunywa maji haya?

Mke wa Kutafuna: Ndio, na ndiyo maana msimu wa kiangazi huwa hatuji mara kwa mara ili kuwapisha wanyama wakali nyakati za jioni kunywa maji.

Chanuo: Makubwa, kweli tembea unyaone.

Chanzo: *Matusi*, onesho la 2, dakika 05:6:14

Mtunzi wa filamu anasawiri mgogoro huo kwa kuonesha mandhari halisi ya watanzania yaliyopo katika vijiji yetu. Pia, mandhari ya shimo la maji yanapatikana katika filamu ya *Matusi* kwenye maonesho kadhaa. Mfano mzuri ni katika onesho la pili kutoka dakika ya 05:40 hadi 7:15.

Pia matumizi ya mapambo pamoja na maleba yanaibua mandhari yenye lengo la kuonesha dhamira ya umasikini uliokithiri katika jamii. Umasikini huo unaonesha uhalisi wa Watanzania. Mtunzi wa filamu hizi amekwepa kutumia gari za kifahari, starehe za hoteli kubwa na gharama za mavazi ya wasani, vitu ambavyo huwa havina uhalisi wa watanzania, sio tu wanaotazama filamu bali hata wanaoigiza filamu hizo. Kwa sababu mavazi na vipando au nyumba za kifahari huwa yamekodiwa. Nyumba hizo huwa hazioneshi maisha ya Mtanzania wa kawaida. Hivyo, hazitatui kero za watanzania. Na kwa maana hiyo, huwa zinakosa thamani ya kifasihi. Katika kuunga mkono hoja hii, Madebe[2] anasema:

> *Kumekuwa na filamu nyingi mpya lakini hakuna filamu bora. Mimi nimeamua kujibainisha kwenye maadili ili kutengeneza ubora. Mimi ndio msanii wa pekee nnayejiongoza mwenyewe, kwenye maadili na lugha ya Kiswahili. Filamu zangu zimekuwa bora kwa sababu filamu zangu ni tofauti na wengine. Waingizaji wengi wanatatizo la ubunifu wa uandishi wa "script" pamoja na matumizi ya lugha. Mimi naweza kufanya vile wanavyovifanya wasanii wengine lakini wao hawawezi. Hawawezi kuyatumia maadili na wakaweza kuwa na filamu kwa sababu wao hawana maadili … utashi wa wandishi wa kutumia maadili unania ya kujitofautisha na wasanii wengine. Mtindo huu unaifanya Sanaa kuwa bora kama asemavyo mtunzi: "Filamu zangu zimekuwa bora kwa sababu filamu ni tofauti na wengine. Waingizaji wengi wanatatizo la ubunifu wa uandishi wa "script" pamoja na matumizi ya lugha".*

Chanzo: Mahojiano ya mtunzi wa filamu ya *Matusi* na Carrymastor Tv

[2] Madebe ni mhusika mkuu wa katika filamu ya Matusi na Wali wangu. Mazungumzo hayo yamefenyika katika chanel ya mtandaoni ya Carrymastor TV.

Maelezo yanaonesha kutumia kwa mandhari halisi ni kuendeleza maadili ya filamu yenyewe. Pia, yanaonesha kuwa wasanii wengi wa filamu hutumia mandhari za zisizo halisi kwa waigizaji wala watazamaji wa filamu hizo. Ubora huu usemwao na mtunzi unaonekana upo kwenye utashi na majigambo, jambo ambalo lina ukweli.

Katika kuthibitisha kuwa maadili yanatoa ubora wa filamu, **[8]** wanasisitiza kuwa maadili ndio kigezo cha msingi cha kuingizwa katika orodha ya filamu bora. Hii ina maana maadili hutazamwa ikiwa filamu hiyo imesawiri mandhari halisi ya walengwa wa filamu hiyo. Wanaongeza kuwa miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na shauku inayoongezeka katika tafiti za maadili yanayooneshwa katika filamu, haswa katika fasihi ya watoto na vijana. Wanaongeza tena kwamba filamu zinazolenga watoto na vijana zinaweza kuwasilisha maadili kwa watazamaji wao. Zaidi ya hayo, sinema hutumika kwa madhumuni ya burudani, elimu na kuitaka jamii iwe na hima katika kujifunza maadili. Hivyo, kutumia kipera cha kimaadili kwa watengenezaji filamu ni kutafuta kutofautisha kazi zao kwa kuchunguza mawazo mapya.

Netflix inazingatia tofauti ya tamaduni. Pia, inakuza usawa wa tamaduni katika uteuzi wa filamu. Netflix inajivunia kuonyesha filamu kutoka tamaduni mbalimbali. Filamu hizo hutazamwa kwa kuzingatia vigezo vingi, vikiwamo maadili na mandhari. Uchunguzi huo hufanya kwa filamu za kidunia ikiwa ni pamoja na filamu za Kiswahili na za Kiafrika. Ted Sarandos (2023)[3] anasema kuwa Netflix imethibitisha kuwa inajali usawa wa tamaduni, na kwamba inazingatia tamaduni na misingi ya kijamii inayohusiana na filamu kutoka sehemu yoyote ya dunia, ikiwa ni pamoja na Afrika. Hii inamaanisha kwamba filamu zinazohusiana na Kiswahili lazima zizingatie muktadha wa tamaduni, na kuepuka maudhui yanayoweza kuathiri tamaduni za maeneo husika.

5.0 Hitimisho na Mapendekezo

Kwa ujumla filamu za Kitanzania zimekuwa na athari kubwa ya kitamaduni kwa kuiga tamaduni za jamii nyingine. Wapo wanaothubutu kuchota lugha, mandhari, mavazi na hata majina ya wahusika wao kuwa ya Kiulaya. Hali hii inapunguza thamani ya filamu hizo. Kwa sababu thamani ya fasihi hutarajiwa kuihusu jamii inayoandikiwa fasihi hiyo. Hivyo, Makala hii inashajiisha utumizi wa thamani ya Mswahili katika filamu za Kiswahili. Katika kuendeleza tamaduni na maadili ya Mswahili serikali inaweza kuandaa utaratibu maalumu wa kutoa tunzo au ruzuku kwa filamu zilizosadifu kulinda na kuendeleza utamaduni wa Mswahili. Aidha, sheria kali za udhibiti wa filamu na utamaduni zinaweza kusaidia kuimarisha kwa filamu za kitamaduni. Pia, vyombo vya Habari vya ndani vijitahidi kuonesha filamu zenye mrengo wa utamaduni wa Mswahili.

6.0 Marejeleo

[1] BAKIZA (2010) Kamusi ya kiswahili fasaha. Oxford univesity press. Nairobi.

[2] Bordwell, D. & Thompson, K. *Film Art*: An Introduction (9th ed.). McGraw-Hill. (2010).

[3] Ted Sarandos ni mkurugenzi mkuu wa maudhui wa Netflix. Ni muongozaji mkuu wa uzalishaji wa maudhui ya filamu zinazopaswa kupewa tunzo au kukubaliwa na Netflix kama filamu bora za kiulimwengu.

[3] Chairina, I. A. "An Analysis of Moral Values in the Movie COCO." *Proceedings of the 2nd English Education International Conference (EEIC) in conjunction with the 9th Annual International Conference (AIC).* Universitas Syiah Kuala, vol. Banda Aceh, Indonesia. (2019) Uk. 62.

[4] Davies, D. "Aesthetics and literature: Londan: Oxford University Press. (2007)

[5] Kasiga, G. A, "Uibukaji wa U- Nigeria katika Tasnia ya Muziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania." Journal of Kiswahili and Other African Languages, (2023). Vol. 1(1),UK. 18 - 30

[6] Lamarque, P, "Aesthetics and literature: a problematic relation? Katika jarida la Philosophical Studies. (2008) Vol 135 (1) uk.85.

[7] Mazrui, A. M na Syambo. B.K (1992) Uchambuzi wa Fasihi.Eduational Publisher.

[8] Miftahuljanah, Z na Sarawat, L(2021) framing moral: A study of moral value in Netfix teen movie findind Ohana (2021 katika htttp//dox.doi.org.10.18522/kssv. Uk.6-9.

[9] Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

[10] Pembe, H. "Majina ya Wahusika katika Fasihi ya Kiswahili". Mulika (2017) Toleo Maalum: Makala ya Kongamano la CHAUKIDU 2016. Dar es Salaam: TATAKI. kur. 98 – 118.

[11] Ponera A S. na. Kessy E. M "Thamani ya Mawasiliano katika Ufyosi wa Jumbe za WhatsApp. Katika jarida Nuru ya Kiswahili, (2022). Juzuu 1(1) Uk 31 – 61.

[12] Ponera, A. S Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi. (2014). Karjamer Printing Technology, Dar es Salam.

[13] Samwel umahiri katika fasihi ya kiswahili: mwongozo kwa mwanafunzi na mwalimu wa fasihi simulizi na andishi (2015). Dar es Salam. Movel Publisher.

[14] Sanga, N. A. "Thamani ya ujumi wa Kiafrika katika hadithi fupi Simulizi za Kiswahili." Katika jarida la MULIKA (2021) Na. 40(1). Uk. 114.

[15] Simiyu, F.W. (2015). Muingiliano tanzu katika fasihi simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu naMwanakogwa. Tasnifu ya sahada ya Uzamifu katika Kiswahili. Chuo kikuu cha Kenyatta

[16] Stecker R. Two Definitions of Artistic Value. (2019) Central Michigan University.

[17] TUKI 2004. Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Pili. Nairobi: Oxford University Press.

[18] Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi. Focus Publication Limited.